# CHETI CHA ELIMU YA MSINGI KENYA (KCBE)
# TATHMINI YA SHULE YA UPILI YA JUU
# KAZI YA ZIADA YA AGOSTI, 2026
# GREDI YA 10 – KISWAHILI
# Muda: Saa 2

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: ______________________________ Shule: ______________________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako katika nafasi ulizopewa hapo juu.
2. Andika jina la shule yako na darasa lako katika nafasi ulizopewa.
3. Andika nambari yako ya usajili na tarehe ya tathmini katika nafasi ulizopewa.
4. Karatasi hii ina sehemu mbili: A na B.
5. Jibu maswali yote katika sehemu A na sehemu B.
6. Jibu maswali kwa lugha ya Kiswahili.
7. Majibu yote LAZIMA yaandikwe katika nafasi ulizopewa kwenye karatasi hii.
8. USIONDOE ukurasa wowote kutoka kwenye karatasi hii ya maswali.

**ALAMA ZA MWANAFUNZI**

| SEHEMU | SEHEMU A | SEHEMU B | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 30 | ALAMA 50 | | 90-100 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI | |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | |

## SEHEMU YA KWANZA: (ALAMA 30)

### Swali la 1: Kusikiliza na Kuzungumza (Alama 10)

*(Mwalimu atamsomea mwanafunzi kifungu kifupi kisha mwanafunzi ajibu maswali yafuatayo kwa sauti/maandishi)*

(a) Taja sauti mbili zinazopatikana katika maneno haya: **Bwawa**, **Mbwa**. (Alama 2)

1. ________________
2. ________________

(b) Wewe ni kiongozi wa wanafunzi katika shule ya **Kiriaini**. Unatakiwa kuwashawishi wenzako kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira. Toa hoja mbili utakazotumia. (Alama 4)

1. ______________________________________________________________
2. ______________________________________________________________

(c) **Mjadala:** "Matumizi ya simu shuleni yana faida kuliko hasara." Toa msimamo wako na sababu moja. (Alama 2)

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

(d) Tofautisha kati ya sauti **/b/** na **/mb/** kwa kutoa mifano miwili ya maneno. (Alama 2)

| sauti **/b/** | sauti **/mb/** |
| --- | --- |
| | |
| **Mifano** | |
| | |
| | |

**Swali la 2: Ufahamu wa Kusoma (Alama 10)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Katika mji wa Eldoret, kulikuwa na kijana mmoja kwa jina Zuma aliyekuwa akisoma katika Shule ya Upili ya Strathmore. Zuma alikuwa mwanafunzi mwenye bidii sana katika masomo yake na alipenda kutumia muda wake mwingi kusoma vitabu mbalimbali. Kati ya masomo yote aliyoyasoma, Kiswahili ndicho kilichomvutia zaidi. Alifurahia kusoma hadithi, riwaya, tamthilia, ushairi na aina nyingine za fasihi simulizi. Kila alipokuwa na muda wa ziada baada ya masomo, angeonekana katika maktaba ya shule akisoma au kutafuta vitabu vipya vya kuongeza maarifa yake.

Siku moja, alipokuwa akifanya utafiti kuhusu tamaduni mbalimbali za jamii za Kenya, aligundua kuwa maktaba ya shule ilikuwa na vitabu vichache sana vya lugha ya Kiswahili. Vitabu vingi vilivyokuwapo vilikuwa vya masomo mengine kama vile Sayansi, Hisabati na Jiografia. Hali hiyo ilimfanya ahuzunike kwa sababu wanafunzi wengi walikosa nafasi ya kusoma vitabu vya ziada vya Kiswahili ambavyo vingewasaidia kuboresha lugha yao, kuongeza msamiati na kukuza uwezo wao wa kufikiri kwa kina.

Baada ya kutafakari kwa muda, Zuma aliamua kutafuta suluhisho la tatizo hilo. Alizungumza na walimu wa Kiswahili pamoja na uongozi wa shule kuhusu umuhimu wa kuongeza idadi ya vitabu vya Kiswahili katika maktaba. Walimu walimpongeza kwa wazo lake na wakamshauri kuanzisha kampeni ya kuchangisha vitabu kutoka kwa wazazi, wanafunzi wa zamani wa shule hiyo na wanajamii waliokuwa tayari kusaidia elimu.

Zuma alianzisha kamati ya wanafunzi iliyokuwa na jukumu la kuhamasisha uchangiaji wa vitabu. Wanafunzi walitengeneza mabango, waliandika matangazo na hata kutumia mitandao ya kijamii kuwafikia watu wengi zaidi. Kampeni hiyo ilipata mafanikio makubwa kuliko walivyotarajia. Baada ya miezi michache, mamia ya vitabu vya Kiswahili vilikuwa vimekusanywa na kuongezwa katika maktaba ya shule.

Kutokana na juhudi hizo, wanafunzi wengi walipata hamu ya kusoma vitabu vya Kiswahili. Matokeo ya somo hilo yakaanza kuimarika, na shule ikajulikana kwa kuwa na mojawapo ya maktaba bora zaidi katika eneo hilo. Zuma alitambua kuwa mtu mmoja mwenye maono na dhamira anaweza kuleta mabadiliko makubwa katika jamii yake. Kitendo chake kilikuwa mfano mzuri wa uongozi, uwajibikaji na kujitolea kwa maendeleo ya elimu.

(a) Eleza jinsi tabia ya Zuma ilivyochangia kuboresha elimu katika shule yake. (Alama 1)

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

(b) Unafikiri ni kwa nini wanafunzi wengi hawakuwa wakisoma vitabu vya Kiswahili kabla ya kampeni ya Zuma? Toa sababu mbili. (Alama 2)

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

(c) Kama ungekuwa mkuu wa shule hiyo, ungechukua hatua gani nyingine ili kukuza utamaduni wa usomaji wa vitabu miongoni mwa wanafunzi? (Alama 2)

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

(d) Je, kampeni ya Zuma ilikuwa na manufaa gani kwa wanafunzi na shule kwa ujumla? Toa hoja mbili. (Alama 2)

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

(e) Ni maadili gani mawili yanayojitokeza kutoka kwa Zuma? Fafanua. (Alama 2)

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

(f) Kwa maoni yako, ni changamoto zipi ambazo Zuma angeweza kukumbana nazo wakati wa kuendesha kampeni ya kuchangisha vitabu? (Alama 2)

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

(g) Ikiwa shule yako ingekuwa na tatizo kama hilo, ungewezaje kushirikiana na wenzako kulitatua? (Alama 2)

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

(h) Tathmini kauli hii: "Mtu mmoja anaweza kuleta mabadiliko makubwa katika jamii." Tumia mifano kutoka kwenye kifungu kuthibitisha jibu lako. (Alama 3)

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

(i) Eleza ujumbe mkuu wa kifungu hiki na umuhimu wake kwa vijana wa leo. (Alama 3)

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

(j) Andika muhtasari wa kifungu hiki kwa sentensi tatu ukionyesha tatizo, suluhisho na matokeo yake. (Alama 4)

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

(c) Toa kisawe cha neno: Kuanzisha. (Alama 1)

____________________________________________________________________________

____________________________________________________________________________

**Swali la 3:** Jaribio la Kujaza Mapengo **(Alama 10)**

*Jaza pengo kwa neno lifaalo zaidi.*

Hapo zamani za kale, palikuwa (1)_________ mzee mmoja aliyekuwa na hekima sana. Aliishi katika kijiji (2)_________ Kilgoris. Kila (3)_________ vijana walipokuwa na matatizo, walimtembelea (4)_________ ushauri. Mzee huyo (5)_________ aliwafunza vijana (6)_________ bidii na heshima. Alisema kuwa (7)_________ ni siri ya mafanikio. Siku hizi, (8)_________ wengi wamesahau maadili ___________(9). Ni muhimu ___________________(10) lugha yetu na utamaduni wetu.

**SEHEMU YA PILI: SARUFI NA INSHA (ALAMA 50)**

**Swali la 4: Sarufi na Matumizi ya Lugha (Alama 30)**

(a) **Aina za Maneno:**

Tambua aina ya maneno yaliyopigiwa mstari. (Alama 4)

"**Yeye** (i) _________ alikimbia **haraka** (ii) _________ kuelekea **shuleni** (iii) _________ na **yule** (iv) _________ rafiki yake."

(b) **Ngeli za Nomino:** Weka nomino hizi katika ngeli zao. (Alama 4)

i. Mtoto: ________
ii. Kiti: ________
iii. Meza: ________
iv. Ufunguo: ________

(c) **Nyakati na Ukanushaji:**

Kanusha sentensi ifuatayo katika wakati uliopita. (Alama 4)

"Mwanafunzi alisoma kitabu jana."

______________________________________________________________________

(d) **Mnyambuliko:**

Nyambua kitenzi **'Soma'** katika kauli hizi: (Alama 4)

i. Kutendea: ________________
ii. Kutendwa: ________________

(e) **Sentensi:** Ainisha sentensi hii (Sahili, Ambatano au Changamano). (Alama 2)

"Mama anapika chakula na baba anasoma gazeti."

______________________________________________________________________

(f) **Viakifishi:**

Sahihisha sentensi hii kwa kutumia herufi kubwa na alama za nukuu. (Alama 4)

"mwalimu alisema, mwanafunzi soma kwa bidii."

______________________________________________________________________

(g) **Isimujamii:**

Taja sifa mbili za **Sajili ya Sokoni**. (Alama 4)

i. ____________________________
ii. ____________________________

(h) **Kinyume:**

Toa kinyume cha maneno haya. (Alama 4)

i. Keti: ________________
ii. Mrefu: ________________

**Swali la 5: Insha (Alama 20)**

*Chagua mada MOJA na uiandikie insha isiyopungua maneno 200.*

1. **Barua ya Kirafiki:** Andika barua kwa rafiki yako anayeishi **Mombasa** ukimweleza kuhusu maisha yako katika shule mpya ya Gredi ya 10.
2. **Insha ya Picha:**



Angalia picha ifuatayo ya soko la **Maasai Market** kisha uandike insha ya masimulizi kuhusu tukio lililotokea hapo.

3. **Insha ya Wasifu:** Mwandikie wasifu mwalimu wako unayempenda zaidi shuleni.

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**MAJIBU YA KISWAHILI GREDI YA 10**

**SEHEMU YA KWANZA**

**Swali la 1: Kusikiliza na Kuzungumza**

***(a)***

1. /bw/
2. /mbw/

***(b)***

1. Kutunza mazingira husaidia kuzuia mmomonyoko wa udongo.
2. Kupanda miti husaidia kuhifadhi mazingira na kuvutia mvua.

***(c)***

Msimamo: Matumizi ya simu shuleni yana faida kuliko hasara kwa sababu yanarahisisha utafiti na kujifunza mtandaoni.

***(d)***

| **Sauti /b/** | **Sauti /mb/** |
|---|---|
| Baba | Mbwa |
| Bata | Mbuni |

**Swali la 2: Ufahamu wa Kusoma**

***(a)***

Tabia ya Zuma ya kuwa mbunifu na mwenye bidii ilisaidia kuongeza vitabu vya Kiswahili na kuboresha elimu shuleni.

***(b)***

1. Maktaba ilikuwa na vitabu vichache vya Kiswahili.
2. Wanafunzi hawakupata fursa ya kusoma vitabu vya ziada vya Kiswahili.

***(c)***

Ningeanzisha klabu ya usomaji wa vitabu na mashindano ya kusoma.

***(d)***

1. Wanafunzi walipata vitabu vingi vya Kiswahili.
2. Matokeo ya Kiswahili yaliboreka.

***(e)***

1. Uongozi – Zuma aliongoza kampeni ya kuchangisha vitabu.
2. Uwajibikaji – alichukua hatua kutatua tatizo la shule.

***(f)***

1. Ukosefu wa vitabu vya kuchangiwa.
2. Baadhi ya wanafunzi kutoshirikiana.

***(g)***

Ningeshirikiana na wenzangu kuandaa kampeni ya kuchangisha vitabu na kuhamasisha usomaji.

***(h)***

Ni kweli. Zuma peke yake aligundua tatizo, akaanzisha kampeni na hatimaye shule ikapata vitabu vingi na matokeo kuboreka.

***(i)***

Ujumbe mkuu ni kuwa mtu mmoja mwenye maono anaweza kuleta mabadiliko makubwa. Vijana wanapaswa kuwa wabunifu na kuwajibika katika jamii.

***(j)***

Tatizo lilikuwa upungufu wa vitabu vya Kiswahili maktabani. Zuma alianzisha kampeni ya kuchangisha vitabu kutoka kwa jamii. Matokeo yake wanafunzi walipata vitabu vingi na matokeo yao yakaboreshwa.

***(k)***

Kisawe cha "Kuanzisha":

- Kuanza
- Kubuni

**Swali la 3: Jaribio la Kujaza Mapengo**

1. na
2. cha
3. mara
4. kupata
5. huyo
6. kuhusu
7. elimu
8. vijana
9. hayo
10. kutunza

**SEHEMU YA PILI**

**Swali la 4: Sarufi na Matumizi ya Lugha**

***(a) Aina za Maneno***

(i) Kiwakilishi

(ii) Kielezi

(iii) Nomino

(iv) Kivumishi

***(b) Ngeli***

i. Mtoto – A-WA

ii. Kiti – KI-VI

iii. Meza – I-ZI

iv. Ufunguo – U-I

***(c) Ukanushaji***

Mwanafunzi hakusoma kitabu jana.

***(d) Mnyambuliko***

i. Somea

ii. Somwa

***(e) Aina ya Sentensi***

Sentensi Ambatano.

***(f) Viakifishi***

Mwalimu alisema, "Mwanafunzi, soma kwa bidii."

***(g) Sajili ya Sokoni***

1. Matumizi ya lugha ya mseto.
2. Matumizi ya vichekesho na utani.

***(h) Kinyume***

i. Simama

ii. Mfupi

**insha**

S.L.P 123,
Nakuru.

30 Agosti 2026.

Rafiki yangu Amina,

Natumai uko salama pamoja na familia yako huko Mombasa. Mimi ni mzima wa afya na ninaendelea vyema na masomo yangu katika shule mpya ya Gredi ya 10.

Shule yangu mpya ni nzuri sana na ina mazingira mazuri ya kujifunzia. Walimu ni wakarimu na wanatufundisha kwa bidii. Nimepata marafiki wengi wapya ambao wananishirikisha katika shughuli mbalimbali za shule.

Pia tuna maktaba kubwa yenye vitabu vingi vya kujisomea. Ninapenda sana kusoma vitabu vya Kiswahili na Sayansi. Shule yetu pia ina viwanja vikubwa vya michezo ambapo hushiriki kandanda na riadha.

Ninafurahia maisha ya shule hii na ninaamini nitafanya vizuri katika masomo yangu. Salamu nyingi kwa wazazi wako na marafiki wote.

Rafiki yako,

Kevin

**Insha**

Mwalimu ninayempenda zaidi shuleni ni Bw. Otieno. Yeye ni mwalimu wa Kiswahili katika shule yetu. Bw. Otieno ana umri wa makamo na ni mtu mrefu mwenye tabasamu la kuvutia.

Ninampenda kwa sababu huwa anafundisha kwa njia rahisi ambayo wanafunzi wote wanaielewa. Huwa na subira anapowaelekeza wanafunzi na yuko tayari kuwasaidia wakati wowote wanapopata matatizo ya masomo.

Mbali na kufundisha, Bw. Otieno ni mlezi mzuri wa wanafunzi. Hutuhimiza kufanya kazi kwa bidii, kuheshimu wengine na kuwa na nidhamu. Pia huandaa mashindano ya mijadala na usomaji wa vitabu ili kuboresha lugha yetu.

Kwa kweli, Bw. Otieno ni mfano bora wa mwalimu anayejitolea kwa maendeleo ya wanafunzi wake. Ninatamani kuwa kama yeye siku zijazo.